

Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga (ERPP)

Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili Zanzibar zinatekeleza mradi huu kwa ufadhili wa Mpango wa Kuendeleza Kilimo na Kuongeza Upatikanaji wa Chakula Duniani (*GAFSP*).

Lengo la mradi ni kuongeza uzalishaji wa mpunga kukidhi mahitaji ya ndani na kupanua mauzo nchi jirani ambapo umejikita katika mifumo endelevu ya mbegu, Kuboresha uzalishaji wa mazao, ubunifu wa masoko na usimamizi na uratibu madhubuti wa mradi.

Kwa upande wa Tanzania Bara, mradi unatekelezwa Mkoa wa Morogoro katika Halmashauri za Wilaya za Kilombero, Kilosa, Mvomero, Morogoro, Malinyi na Ulanga wakati Zanzibar unatekelezwa katika skimu za umwagiliaji za Kibonde Mzungu, Mtwango, Koani, Mchangani, Bandamaji (Unguja), Machigini, Kwalempona, Ole, Dobi - 1 na Dobi - 2 (Pemba).

Mradi huu umewezesha kuongezeka kwa tija katika zao la mpunga kutoka tani 1.8 kwa hekta mwaka 2012/2013 mpaka tani 4.6 mwaka 2016/2017 na wakulima 7100 wamepata mafunzo ya kilimo cha shadidi (*SRI*).

Kupitia kamati yake ya uendeshaji, *GAFSP* ilikubali kuipatia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kiasi cha Dola za Kimarekani Milioni 22.9 kwa ajili ya kutekeleza mradi huu kwa muda wa miaka mitano (2015-2020).